# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL2

# KISWAHILI PAPER 2 QUESTIONS

## 1. UFAHAMU (Alama 15 )

### Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali

Mahali ni nyumbani katika chumba cha mapokezi. Pana makochi kochokocho ya bei. Wasikika mlio wa gari linalopunguza mwendo na kusimama nje, zii, isipokuwa muziki murua. Milango ya gari inasikika ikifunguliwa. Muziki unanyamaza. Milango inafungwa.

SAFARI: (Anafungua mlango wa nyumba na kumkaribisha ndani nwenzake). Karibu ndani mpenzi.

REHEMA: (Akiingia huku yuafuta jasho kwa kitambaa). Ahsante. (Akitembeza macho kwa kukiangazia chumba chote). Lo! Jamani.

SAFARI: (Akimtazama). Nini mpenzi ?

REHEMA : Kweli nyinyi ndio mnajua maana ya sitting room.

SAFARI: Acha bwana we. Sinivishe kilemba cha ukoka. Kiti hicho. Unakiaibisha. Kaa tafadhali.

REHEMA : (Akiketi). Ahsante. (Anajiopea. Safari anafungua muziki taratibu. Anachukua glasi na kumwekea Rehema kijimezani mbele yake. Anammiminia maji ya machungwa kutoka frijini. Yeye pia anachukua glasi yake na kujaza. Anaketi kando kidogo. Kila mmoja anapiga funda. Safari anamtazama mwenzake). Je, mwanao hajambo?

SAFARI: Achana naye huyo bwana. Ah! Anyway. Ok. Haidhuru. Samahani.Kwanza ni vizuri umenielekeza moja kwa moja kwenye sababu ya kukutana kwetu hapa nyumbani.

REHEMA: Ehe!

SAFARI: Rehema mpenzi tumejuana kwa muda wa kutosha sasa; na kama ujuavyo mazoea...

REHEMA: Nakubaliana nawe.

SAFARI: Tukiendelea hivi tutakuja kuwa mtu na dadake, ambaye siyo madhumuni. (Akimkaribia). Baada ya muda wote huu, si vibaya tukielewana kabisa kabisa. Ndiyo sababu nikakuleta nyumbani ili upajue na tuzungumze kwa makini pasina kusumbuliwa.

REHEMA: Sawa.

SAFARI: Ningetaka tuelewane kwa sababu(Akimkumbatia) naamini tunaweza kuelewana. Ama vipi Rehema?

REHEMA: Sawa

SAFARI: Kutojuana na kutoelewana ifaavyo kimbele kunaweza kusababisha maisha ya wasiwasi na kutoaminiana kati yetu baadaye.

REHEMA : (Sauti ya chini) Kweli.

SAFARI: Ndiyo sababu sikusita kukujulisha hali yangu mara tu baada ya kujuana nawe.

REHEMA: Samahani. Hata mimi pia ningejijulisha kwako barabara wakati huo huo.

SAFARI: Usijali. Wahenga husema, "Chelewa ufike" Ulilokosa kunieleza wakati huo waweza kunieleza sasa. Siyo?

REHEMA: (Sauti ya mbali, akigoboa vidole). Ndiyo. lakini kuna jambo moja ambalo ningetaka tuelewane kwanza.

SAFARI: Nieleze tu mpenzi. Siwezi kushindwa kukuelewa. Niamini. Sema usiogope.

REHEMA: Halikuwa kosa langu. Samahani sana Safari mpenzi.

SAFARI: (Akimsikiliza kwa makini) Usinishangaze Rehema. Ni kosa gani hili ambalo halikuwa lako?

REHEMA : (Akijibanza kwa safari). Kwa ufupi mpenzi kama wewe, mimi pia...

SAFARI: (Akijivuta). Una mtoto Rehema !

a) Taja mambo manne yanayodhihirisha kuwa safari ni mtu anayejiweza. (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
b) Kwa nini hasa Safari alimpeleka Rehema nyumbani kwake? (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
c) Kwa nini Rehema aliharakisha kumwuuliza Safari kuhusu mwanaye? (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
d) Rehema anatupiwa maneno…" kama ujuavyo mazoea…" Anajibu, "Nakubaliana nawe"
Eleza sababu ya kukubaliana haraka. (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
e) Jamii ya sasa inamchukuliaje mtoto aliyezaliwa nje ya ndoa? (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
f) Fafanua ukweli wa methali, "Nyani haoni kundule." Kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)
……………………………………………………………………………………………………….
……………………………………………………………………………………………………….
g) Eleza maana ya maneno / vifungu vya maneno haya kama yalivyotumika katika habari. (alama 3)
i. Kumvisha kilemba cha ukoka.
……………………………………………………………………………………………………….
ii. Tuliagana
……………………………………………………………………………………………………….
iii. Kwa dhati
……………………………………………………………………………………………………….

## 2. UFUPISHO (Alama 15 )

### Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali

Sote tuna wajibu kudumisha na kuimarisha usalama barabarani. Hili linatokana na ukweli kuwa maendeleo ya kiuchumi ya nchi hutegemea sana mawasiliano kwa njia ya barabara. Licha ya maendeleo makubwa ya kiteknolojia yaliyokwisha kushuhudiwa, watu bidhaa na huduma nyingi zingali zinaegemea usafiri kwa njia ya barabara.

Kutokana na hali hii, ni dhahiri shahiri kuwa kuimarisha usalama barabarani ni kuchangia kuleta maendeleo nchini. Kila mwaka nchi hupoteza idadi kubwa ya wananchi, rasilmali muhimu zaidi, kupitia kwa ajali za barabarani au bora tuseme kwa kukosekana usalama barabarani. Hasara kubwa kiuchumi hutokea, inapobidi magari kukarabatiwa au mengine kununuliwa ili kuchukua nafasi ya yaliyoharibika kabisa. Usalama barabarani unapodumishwa rasilimali zaidi huweza kusambazwa kwenye sekta zingine muhimu.

Inapobidi kuchunguzwa chanzo cha kukosekana kwa usalama barabarani, kidole cha lawama hutoa hali duni za barabarani. Tafakuri zitatukosoa na kutoa lawama kwa binadamu. Kama barabara imejengwa vibaya wa awali kulaumiwa ni binadamu. Utunzaji na ukarabati ukiwa duni basi wa kushutumiwa ni binadamu. Ajali itokeapo akengemekwe mwanadamu kwani ndiye mwendeshaji gari.

Ni bayana kuwa watumiaji wa barabara huhusika na kukosekana kwa usalama barabarani.

Watembeao kwa miguu huweza kuhatarisha usalama wao na wengine wanapovuka barabara kusikofaa au kutembea barabarani kwenyewe.
Kunao hasa mjini wanaozumbua riziki kwa kusukuma rukwama. Baadhi yao hukosa kufuata mkondo sahihi na hivyo huwatatiza watumiaji wengine. Nako katika maeneo ya mashambani, waendeshaji baiskeli huwa ni tatizo. Wao hukatalia barabarani licha ya kupigiwa honi kwa imani kuwa madereva wanawaona. Hitilafu ndogo ikitokea aghalabu wa kuhasirika ni mwendeshaji baiskeli.

Pikipiki za kubeba abiria maarufu kama "bodaboda" zimekuwa vivutio vikubwa. Moja ya sababu za kupendeka ni kwamba humpeleka abiria hadi sebuleni mwake. Ni njia nzuri ya kusafiri laiti ingedhibitiwa. Abiria wengi wa "bodaboda" wamelemaa na wengine kupoteza maisha yao kutokana na ajali hizi " za bodaboda". Mashine haina lawama kamwe! waendeshaji ndio wa kulaumiwa. Baadhi hawajapata mafunzo mwafaka kuhusiana na uendeshaji wa pikipiki. Imani potovu inayotawala ni, ' nishaimudu baiskeli, pikipiki si kitu!'

Kundi lingine linalopaswa kuangaziwa ni madereva, wawe wa magari ya kibinafsi, magari ya abiria au magari ya uchukuzi wa mizigo. Uendeshaji wa kasi, upakiaji kupita kiasi wa abiria au mizigo huhatarisha usalama barabarani. Kunao madereva ambao huchokora vidhibiti mwendo ili waweze kuendesha magari kwa kasi zaidi. Wengine hujishughulisha na mambo yanayoweza kuathiri makini ya uendeshaji kama vile kutumia rununu. Jambo hili licha ya kuwa kinyume cha sheria ni hatari mno. Madereva wanapohiari kuendesha magari mabovu basi wanapaswa kulaumiwa.

Wamiliki hasa wa magari ya usafiri wa umma nao wana sehemu yao. Katika harakati zao za kuulinda uwekezaji na kupata faida kutoka kwa mtaji wao, hupuuza utunzaji wa magari kwani una gharama. Zaidi ya hayo, wao huwashinikiza wahudumu kwenda kasi ili kuwahi safari nyingi na hivyo kuzidisha faida. Bila shaka hali huhatarisha usalama barabarani.

Kufikia hapa itaelekea ni kama hakuna afueni. Ukweli ni kwamba hali hii ya kukatisha tamaa inaweza kubadilishwa. Zipo idara ambazo zimepewa majukumu ya kusimamia masuala ya usalama barabarani,.Askari wa trafiki wanapaswa kuwa mstari wa mbele. Uadilifu katika utenda kazi wao utachangia sana katika kuimarisha na kudumisha usalama barabarani. Mambo ya ' leta leseni' kila uchao hayasaidii chochote. Taasisi
zinazotoa mafunzo ya udereva zitayarishiwe mtaala mwafaka ili kuhakikisha apewaye leseni amefundishwa ipasavyo. Udereva ni zaidi ya kulisogeza gari mbele tu.

Ukaguzi mkamilifu wa magari ufanywe katika mihula ifaayo. Wamiliki magari nao wahamasishwe juu ya umuhimu wa ukaguzi sahihi. Waone haja ya kuyapeleka magari yao kukaguliwa mara kwa mara. Mashirika ya bima na washikadau wengine wahimizwe kutoa vihimizo. Gharama za bima na bei za vipuri zinaweza kupunguzwa.

Kwa watu binafsi itakuwa bora kuepuka matendo yanayohatarisha usalama barabarani. Abiria wasiingie magari yaliyokwishajaa. Aidha, wasikubali magari kuendeshwa kwa kasi.

a) Eleza mambo yanayozisababisha ajali za barabarani na jinsi yanavyosababisha. (maneno 90 – 100)

**MAANDALIZI**

.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................
.................................................................................................................

**NAKALA SAFI**

.................................................................................................................

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

b) Kwa kuzingatia aya mbili za mwisho onyesha mapendekezo yaliyotolewa kuhusu hatua za kuchukuliwa kupunguza ajali barabarani. (maneno 25 – 30)

**MAANDALIZI**

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

**NAKALA SAFI**

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

## 3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40 )

a Taja aina mbili kuu za sauti kisha uzitolee mfano mmoja mmoja.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

b

Ziweke nomino hizi katika ngeli zake kisha useme ni za aina gani.

i. Huzuni

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

ii. Uji

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

c i. Eleza maana ya kirai. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

ii. Bainisha virai katika sentensi ifuatayo.
Niliwaona wezi hao kando ya barabara. (alama 2)

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

d Yakinisha sentensi ifuatayo.
Sikumwona simba mwenye watoto.

………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………

e i. Mofimu ni nini. (alama 1)

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
ii. Onyesha viambishi awali na viambishi tamati katika neno hili.
Walionana (alama 2)
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

f Andika katika usemi wa taarifa.

"Sikuenda sokoni leo ila nitaenda kesho." Akamjibu.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

g Onyesha matumizi mawili ya mshazari.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

h h) Andika sentensi ifuatayo katika hali isiyodhihirika.
Kipanga hula kuku.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

i Tunga sentensi ukitumia kiwakilishi cha pekee – ingineo katika ngeli ya KI-VI umoja.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

j Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendwa.
Mwenyeji huyo alimpokea mgeni wake leo alfajiri.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

k Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya sabuni na zabuni.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

l Geuza sentensi ifuatayo katika hali ya kinyume.
Watu wengi hupenda pesa.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

m Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali.
Nilimwona mamba niliyemwogopa mno majini.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

n Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi.
Mwalimu alimwandikia mhariri barua vizuri sana kwa kalamu ya mate.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

o Ainisha matumizi ya kiambishi "ji" katika sentensi.
Jino la jitu hilo liliwezesha kujilia chakula kingi kuliko mkimbiaji yule.
………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………………

p Eleza maana ya nahau hii. Piga kamsa.
………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………

q Andika maana mbili za neno: Kina

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

r Eleza maana mbili za sentensi ifuatayo.

Waite watoto wale.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

s Andika methali inayoafiki maelezo haya.
Mtu anayelalamika kuhusu mambo yasiyomhusu ndewe wala sikio.

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

## 4. ISIMUJAMII: (Alama 10 )

a) Fafanua maana ya istilahi zifuatazo: (alama 3)

i. Krioli

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

ii. Misimu

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

iii. Lugha mwiko

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………

b) Eleza huku ukitoa mifano mwafaka sifa saba za sajili ya siasa. (alama 7)

……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………